**HOTUBA YA MHE. *KAPT (MST)* GEORGE H. MKUCHIKA (MB), WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWENYE UFUNGUZI WA KONGAMANO LA KUADHIMISHA SIKU YA MAADILI NA HAKI ZA BINANDAMU, UKUMBI WA PIUS MSEKWA-BUNGENI, DODOMA - TAREHE 11 DESEMBA 2019**

---

*Mheshimiwa Dr. Mary M. Mwanjelwa – Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora;*
*Mheshimiwa Prof. Adeladus Kilangi - Mwanasheria Mkuu wa Serikali;*
*Dkt. Moses Kusiluka - Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu;*
*Mheshimiwa Jaji Mstaafu Harold Nsekela – Kamishna wa Maadili;*
*Bw. Charles Kichele - Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;*
*Mheshimiwa Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu – Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;*
*Brigedia Jenerali John Mbungo - Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU;*
*Mheshimiwa Balozi Dkt. Marten Lumbanga – Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu;*
*Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu Mliopo;*
*Wakuu wa Taasisi za Serikali na Viongozi Wote Mliopo Hapa;*
*Washiriki Wote;*
*Mabibi na Mabwana.*
Habari za asubuhi.

1. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutajalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo kwa ajili ya kuadhimisha siku hii muhimu, **Siku ya Maadili na Haki za Binadamu**. Kwa kuwa siku hii inaadhimishwa kwa kongamano linalowaleta pamoja watumishi wa umma, na mimi Waziri mwenye dhamani ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ningependa kutumia nafasi hii kuwakaribisheni wote katika kongamano hili muhimu.

   Aidha, napenda kuwashukuru Viongozi na Watumishi wa taasisi zote zilizohusika kwa namna moja au nyingine katika maandalizi ya maadhimisho haya.

2. **Ndugu Washiriki,** kama tulivyoambiwa, kaulimbiu ya maadhimisho haya ya ni **"Maadili katika Utumishi wa Umma ni Nguzo Muhimu katika Kuimarisha Utawala Bora na Haki**

**za Binadamu".** Kaulimbiu hii imebeba ujumbe muafaka kwa ajili ya siku hii muhimu. Ninafahamu pia kwamba hata mada zitakazowasilishwa na kujadiliwa leo zimejikita katika kaulimbiu hii. Ni imani yangu kwamba mada hizi pamoja na mjadala utakaofanyika zitajielekeza katika kuwafanya washiriki wa kongamano hili kujitafakari na kuboresha mienendo yao katika utumishi wao.

3. Uzito wa kongamano hili pia unaojionyesha kupitia mada tatu zitakazowasilishwa pamoja na umahiri wa watoa mada. Sote tunamfahamu Balozi *Dkt.* Marten Lumbanga - Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Jaji Mstaafu Harold Nsekela - Kamishna wa Maadili na Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu - Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Wote hawa ni Viongozi wenye uzoefu wa miaka mingi katika utumishi wa umma na ni watu makini sana. Kwa kifupi, ukiwatazama watoa mada unawaona Viongozi waadilifu na wenye weledi mkubwa katika maeneo mbalimbali. Ni imani yangu kubwa kwamba kila mshiriki atuitumia fursa hii kuchota ujuzi na maarifa kutoka kwa Viongozi hawa. Ni imani yangu pia kwamba haya mtakayoyapata leo kutokana na mada hizi yatawachochea kuleta mabadiliko sehemu zenu za kazi.

4. **Ndugu Washiriki,** sote tunafahamu jinsi ambavyo Serikali, hususan Serikali hii ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** inavyosimamia maadili katika utumishi wa umma. Katika kipindi cha miaka minne tumeshuhudia mabadiliko makubwa katika utumishi wa umma. Kiwango cha uadilifu katika utumishi wa umma kimeongezeka kwa kiasi kukubwa. Hivyo, ninapenda kutumia nafasi hii kuwapongeza watumishi wote ambao wameitikia wito wa Serikali wa kuzingatia maadili katika utumishi wa umma.

5. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya watumishi ambao bado wanakiuka msingi ya uadilifu, na wamekuwa wakisababisha usumbufu kwa wananchi na kuharibu taswira ya Serikali. Ningependa kutumia nafasi hii kuwaonya watumishi hao kuacha tabia hiyo. Serikali haitakuwa tayari kuwavumilia watumishi wa aina hii. Aidha, ningependa kuzikumbusha mamlaka za ajira kutosita kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi wote wasiozingatia maadili katika utendaji wa kazi zao.

6. **Ndugu Washiriki,** tukirejea kaulimbiu ya maadhimisho haya tunaona kwamba **maadili** ndilo neno la msingi. Hivyo, ningependa kwa kifupi, kubainisha juhudi mbalimbali ambazo Serikali imeshazichukua katika kuhakikisha kwamba utumishi wa umma unazingatia maadili. Miongoni mwa jitihada za Serikali ni pamoja na kutunga sheria mbalimbali zinazosimamia wa utendaji katika Utumishi wa Umma kama vile **Sheria Na. 13 ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma**, na miongozo mingine ya kiutumishi ambayo imekuwa ikitolewa mara kwa mara.

7. Aidha, kumekuwa na programu mbalimbali za maboresho zikiwemo **Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma, Programu ya Maboresho katika Usimamizi wa Fedha za Umma, Programu ya Maboresho katika Serikali za Mitaa, na Programu ya Maboresho katika Sekta ya Sheria**. Kadhalika, Serikali imekuwa ikihimiza kufanyika kwa Mabaraza ya Wafanyakazi ambayo yapo kwa mujibu wa Sheria, kwa ajili ya kuwapatia fursa watumishi wa umma kueleza kero na matatizo yao sehemu zao za kazi. Vilevile, baadhi ya ofisi za umma zimeanzisha madawati ya kushughulikia malalamiko ya wananchi. Hizi ni baadhi ya juhudi za Serikali katika kujenga utumishi wa umma unaozingatia ufanisi, uwajibikaji, uadilifu, utawala bora. Hizi ni nguzo muhimu katika utoaji wa huduma, hususan katika sekta ya umma.

8. Katika kuimarisha uadilifu katika sekta ya umma, Serikali pia inatekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpangokazi wake ambapo taasisi zote za umma zinapaswa kuwa na **Kamati za Kusimamia Uadilifu**. Mkakati huu ulizinduliwa tarehe 10 Desemba, 2016 na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwenye maadhimisho ya **Siku ya Maadili na Haki za Binadamu.** Mkakati huu ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 01 Julai, 2017. Malengo mahsusi makuu ya Mkakati huu ni:-

    i. Kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa utoaji wa huduma katika sekta ya umma na sekta binafsi;

    ii. Kuwa na ufanisi katika utekelezaji wa mikakati ya mapambano dhidi ya rushwa;

    iii. Kuzijengea uwezo taasisi simamizi za masuala ya utawala bora; na

iv. Kuwa na Uongozi wa Kisiasa madhubuti unaoshiriki kwa dhati katika mapambano dhidi ya rushwa.

Kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Mkakati huu umejikita kwenye sekta za kimkakati zikiwemo **manunuzi ya umma, ukusanyaji wa mapato, utoaji wa haki, maliasili na utalii, madini, nishati, mafuta na gesi, afya, elimu na ardhi.** Mkakati huu unatekelezwa katika ngazi ya kijiji/mtaa, kata, tarafa, wilaya, mkoa na taifa.

9. Ningependa kuchukua fursa hii kuziagiza taasisi zote za umma nchini kusimamia utekelezaji wa Mkakati huu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba kila taasisi inakuwa na **Kamati ya Kusimamia Uadilifu** ili kuweza kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Mkakati huu.

10. Sote ni mashahidi wa jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais wetu, *Dkt.* John Pombe Joseph Magufuli, amekuwa kila mara akionyesha kwa vitendo kutokuvumilia watendaji wabovu Serikali. Wananchi wameonyesha kufurahishwa sana na juhudi na msimamo wa Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake katika kusimamia maadili katika utumishi wa umma. Umakini na uharaka wa Serikali katika kuchukua hatua dhidi wa watumishi wasiozingatia maadili sio tu umeongeza ufanisi kazini bali pia umeongeza imani ya wananchi kwa Serikali yao.

11. Ninapenda kutumia fursa hii kuwaagiza Viongozi wote katika utumishi wa umma kusimamia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi ili kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha utumishi wa umma ili wananchi waweze kupatiwa huduma bora na bila usumbufu wa aina yoyote. Aidha, ningependa kuwaagiza watumishi wa umma wote kutekeleza majukumu yenu kwa kuzingatia maadili na weledi wa taaluma zao wakiongozwa na sheria, kanuni, taratibu na miongozi iliyopo na itakayotolewa.

12. Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, ningependa kuwakumbusha waandaji wa kongamano hili kuniletea muhtasari wa masuala muhimu yatakayotokana na mada zitakazowasilishwa leo pamoja na majadadiliano ili kama kutakuwa na masuala ambayo

yatahitaji hatua za Serikali tuweze kuyafanyia kazi. Na kwa masuala ambayo mtakubaliana kuyatekeleza wenyewe, yatekelezeni ili wakati wa kuadhimisha siku kama ya leo mwakani kila taasisi iweze kutoa taarifa juu ya jinsi ambavyo imetekeleza majukumu yake.

13. Baada ya kusema hayo, naomba nirudie tena kuwakaribisha wote kwenye kongamano hili pamoja na kutoa wito kwa washiriki wote kutumia fursa hii kikamilifu. Kwa haya machache, sasa ninayo furaha kutamka kwamba KONGAMANO LA KUADHIMISHA SIKU YA MAADILI NA HAKI ZA BINADAMU MWAKA 2019 limefunguliwa rasmi.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza.**